
2. UTUKUFU - MISA KARIOBANGI

Mak'Okeyo





UTUKUFU

Utukufu juu kwa Mungu,
Utukufu juu Mbinguni
Na amani kote duniani,
kwa wenye mapenzi mema

1. Tunakusifu tunakuheshimu, tunakuabudu tunakutukuza
Twakushukuru kwa ajili, ya utukufu wako mkuu

2.Ewe Mungu ndiwe mfalme, wa mbinguni Baba Mwenyezi
Ewe Bwana Yesu Kristu, wa pekee mwana wa baba

3.Ewe Yesu Mwanakondoo, wa- Mungu mwana wa Baba
Ewe mwenye kuziondoa, dhambi zetu tuhurumie

4.Ewe mwenye kuziondoa, za dunia dhambi za watu
Ewe mwenye rehema nyingi, upokee maombi yetu

5.Uketiye kuume kwake, Mungu Baba tuhurumie
Kwa kuwa ndiwe uliye, peke yako Mtakatifu

6.Peke yako ni wewe Bwana, peke yako Bwana Mungu
Peke yako ni Mkombozi, peke yako Yesu Kristu

7.Naye Roho Mtakatifu, katika utukufu wake
Mungu mmoja anayeishi, na kutawala milele yote